East African Journal of Swahili Studies, Volume 3, Issue 1, 2021
Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367




**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 3, Issue 1, 2021**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Msatakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda

*Florence Abuyeka Miima, PhD[1] & Vincent Ferrel Kawoya[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S.L.P 43884-0100, Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: miimaflo@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*27 Juli 2021*

**Istilahi Muhimu**:

*Msatakabala, Changamoto, Lugha, Kiswahili, Uganda.*

**IKISIRI**

Kiswahili ni lugha ya kimataifa na ni mojawapo ya lugha rasmi za Muungano wa Nchi za Afrika. Vilevile, katika nchi za Afrika Mashariki, Kiswahili kina hadhi ya aina ya kipekee kikilinganishwa na lugha zingine zenye asili ya Kiafrika. Nchini Kenya na Tanzania ni lugha ya taifa na rasmi. Kwa upande mwingine, nchini Uganda, Kiswahili kinatambulika kikatiba kama lugha ya pili rasmi. Hali kadhalika katika kanda ya maziwa makuu kinategemewa sana kama chombo muhimu cha kufanikisha harakati za kibiashara. Kutokana na ukweli huu kuhusu hadhi na umuhimu wa lugha ya Kiswahili, ingetarajiwa kuwa Kiswahili kingetumiwa kwa mawasiliano rasmi na katika ngazi mbalimbali za kimataifa. Hata hivyo, ni wazi kwamba kinakabiliwa na changamoto chungu nzima hasa zaidi nchini Uganda kiasi kwamba hatima yake haijulikani. Makala hii itaangazia hali ya lugha ya Kiswahili, changamoto zinazoikabili na hatima yake nchini Uganda. Itatoa mapendekezo kuhusu mikakati inayoweza kutumiwa ili kutamanisha wananchi wa Uganda kukienzi Kiswahili, kuinua hadhi yake na kukistawisha ipasavyo.

**APA CITATION**

Miima, F. A. & Kawoya, V. F. (2021). Msatakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda. *East African Journal of Swahili Studies*, *3*(1), 70-77. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367.

**CHICAGO CITATION**

Miima, Florence Abuyeka & Vincent Ferrel Kawoya. 2021. "Msatakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda". *East African Journal of Swahili Studies* 3 (1), 70-77. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367.

**HARVARD CITATION**

Miima, F. A. and Kawoya, V. F. (2021) "Msatakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda", *East African Journal of Swahili Studies*, 3(1), pp. 70-77. doi: 10.37284/eajss.3.1.367.

**IEEE CITATION**

F. A. Miima, & V. F. Kawoya, "Msatakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda", *EAJSS*, vol 3, no. 1, pp. 70-77, Jul. 2021.

**MLA CITATION**

Miima, Florence Abuyeka & Vincent Ferrel Kawoya. "Msatakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 3, no. 1, Jul. 2021, pp. 70-77, doi:10.37284/eajss.3.1.367.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367

## UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ya kimataifa na ni mojawapo ya lugha rasmi za Muungano wa Nchi za Afrika. Vilevile, katika nchi za Afrika Mashariki, Kiswahili kina hadhi ya aina ya kipekee kikilinganishwa na lugha zingine zenye asili ya Kiafrika (Msanjila, 2009). Nchini Kenya na Tanzania ni lugha ya taifa na rasmi. Nchini Uganda, Kiswahili kinatambulika kikatiba kama lugha ya pili rasmi (Mbaabu,1978). Hali kadhalika, katika kanda ya maziwa makuu kinategemewa sana kama chombo muhimu cha kufanikisha shughuli za kibiashara. Nchini DRC, Kiswahili ni miongoni mwa lugha nne za kitaifa. Lugha hizi ni pamoja na Lingala, Kikongo na Chiluba. Haya ni kwa mujibu wa waandishi mbalimbali kama Kihore (1983), Mazrui (1995) na Msanjila (2009).

Kutokana na ukweli huu kuhusu hadhi na umuhimu wa lugha hii, ingetarajiwa kuwa Kiswahili kingepewa uzito unaostahili kwa kutumiwa kwa mawasiliano rasmi katika ngazi mbalimbali za kitaifa kama vile kielimu, bungeni, mahakamani, sherehe za kitaifa, katika shughuli za kibiashara na kadhalika. Ingawa wataalam wengi wa Kiswahili kama vile Whitely (1969), Abdallah (1977), Kihore (1983), Chimera (1998), Mbaabu (1995), Msanjila (1997 & 2003) na wengine wengi wameshughulikia na kutoa mapendekezo kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili kutumika katika hali na nyanja mbalimbali Afrika na hata mataifa mengine, ni wazi kwamba kinakabiliwa na changamoto chungu nzima hasa zaidi nchini Uganda kiasi kwamba hatima yake haijulikani.

Makala hii itaangazia hali ya lugha ya Kiswahili, changamoto zinazoikabili na hatima yake nchini Uganda. Itatoa mapendekezo kuhusu mikakati inayoweza kutumiwa ili kutamanisha wananchi wa Uganda kukienzi Kiswahili, kuinua hadhi yake na kukistawisha ipasavyo.

### Hali ya Kiswahili Nchini Uganda

Kiswahili kiliingia Uganda mnamo miaka ya 1840 kupitia wafanyibiashara Waswahili na wa Kiarabu. Hata hivyo hakijakita mizizi nchini Uganda kinyume na kama ilivyo nchini Tanzania na Kenya. Kuna sababu mbalimbali zinazochangia hali hii ambazo baadhi yazo ni za kisiasa, kijamii na kiisimu. Miongoni mwa sababu za kisiasa ni ukosefu wa sera wazi na mikakati madhubuti ya utekelezaji. Hali hii ilianza wakati wa enzi za ukoloni. Kwa mfano; mnamo mwaka wa 1927, Gavana W. T. *Gowers* alinuia kukifanya Kiswahili kutumika kama chombo cha kufundishia na kutoa huduma za kiutawala nchini Uganda. Ingawa nia yake ilikuwa ni kukikuza na kukieneza Kiswahili kama *Lingua Franca* nchini Uganda, mapendekezo yake yalikuwa na upungufu fulani.

Mapendekezo yake hayakuhusisha makabila makuu ya Kibantu kama vile Watoro, Wanyankole, Wasoga na Waganda. Wakati wa utawala wa Idi Amin mnamo mwaka wa 1973, Kiswahili kilitangazwa kama lugha ya kitaifa nchini Uganda. Hata hivyo tangazo hili halikufuatwa na sera na mikakati ya kulitekeleza. Hatua wazi iliyochukuliwa, ilikuwa tu kuanzisha usomaji wa taarifa ya habari kwa Kiswahili katika runinga na redio za kitaifa.

Kiswahili kilipoingia Uganda, kilihusishwa na watu wa hadhi ya chini kwa mfano, vibarua waliowahudumia Wahindi. Kwa sababu hii, Kiswahili kilichukuliwa kuwa lugha duni iliyotumiwa na watu duni. Jambo hili kwa kiasi fulani limechangia kuwepo kwa mwelekeo hasi hasa kutoka kwa wazungumzaji wa jamii za Kibantu. Kiswahili nchini humo pia kilichukuliwa kama lugha ya wahuni, makahaba, wanyanyasaji miongoni mwa maovu mengine. Kwa sababu ya maovu haya, watu wengi hawakutaka kujinasibisha na Kiswahili. Kwa mfano, wakati wa enzi za utawala wa Obote na Idi Amin, wanajeshi walitumia Kiswahili kuwanyanyasa na kuwatisha raia nchini humo. Kwa hivyo, Kiswahili kilichukuliwa kuwa lugha ya vitisho na kwa hivyo kupelekea kuwafanya raia wengi kuwa na mwelekeo hasi dhidi yake.

Kiswahili pia kilipingwa na Wamishonari hasa katika elimu na shughuli za kidini. Wamishonari walishikilia kwamba njia bora ya kueneza na kuelewa neno la Mungu ni kupitia lugha za Kienyeji. Kwa kuwa Kiswahili si lugha ya Kienyeji, matumizi yake yalipingwa mno na Wamishonari waliohofia kwamba matumizi ya Kiswahili yangechangia katika uenezaji wa Uislamu kwa kuwa, kulingana nao, Kiswahili kilifungamana na Uislamu; na lengo lao hasa lilikuwa ni kufisha dini ya Kiislamu nchini humo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367

Katika ufalme wa Buganda, Kiswahili kilichukuliwa kama lugha ya Kigeni ambayo ilitisha kuhujumu Luganda (lugha ya Baganda). Wakazi wa Buganda wanaenzi sana utamaduni wao na walionelea kwamba kukikubali Kiswahili ingekuwa njia mojawapo ya kuzorotesha utamaduni na utambulisho wao wa kijamii. Mtazamo huu haujabadilika sana. Bado kuna baadhi ya watu ambao wanakiona Kiswahili kama tisho na hatari kwa Luganda.

Hata hivyo, matatizo hayo hayajazuia kabisa uwepo wa Kiswahili nchini Uganda. Katika nyanja ya elimu, Kiswahili kinafundishwa kama somo katika baadhi ya vyuo vikuu kama Chuo kikuu cha Makerere, Kyambogo na kile cha Kiislamu cha Mbale Uganda. Kiswahili pia kinafundishwa katika vyuo vya ualimu nchini humo. Baraza la mitihani (UNEB) linakitambua Kiswahili kama lugha inayotahiniwa katika shule za upili kidato cha nne na sita. Wizara ya Elimu na Michezo (2012) ilipendekeza pia Kiswahili kiingizwe kwenye mtaala wa shule za msingi hasa katika darasa la saba.

Kiswahili vile vile kinatumiwa kwa kiasi fulani katika vipindi vya redio na runinga. Mifano ni *redio Uganda (UBC*), *Pearl FM,* shirika la *Royal Media-Citizen, WAVA TV* miongoni mwa mengine. Kiswahili pia kiliwahi kutumiwa magazetini kama vile gazeti la Mkombozi, Habari za *Uganda Polisi*, *Lulu ya Afrika* na lile la *Mwenzako*. Magazeti hayo yalikuwa tu ya muda na kutoweka kwa kuwa wasomaji hawakuwepo. Vile vile, nyimbo za Kiswahili huchezwa katika vipindi vya redio. Shirika la UBC hutoa mafunzo katika Kiswahili.

Kiswahili kinatumiwa kwa kiasi fulani katika shughuli za kidini; kwa mfano baadhi ya nyimbo za kuabudu zinaimbwa kwa Kiswahili hasa kwa dini ya Kikatoliki ambapo nyimbo kama ***mwanakondoo wa Mungu***, zinasikika mara kwa mara. Kupitia nyimbo hizi, watu wengi hupata fursa ya kusikia Kiswahili na kuanza kujenga hazina ya maneno ya Kiswahili. Vile vile, baadhi ya wasanii hutunga na kuimba nyimbo zao katika lugha ya Kiswahili, kwa mfano, msanii Chameleone, Juliana miongoni mwa wengine. Vile vile vyombo vya utangazaji kama vile Shirika la Citizen linapeperusha vipindi vya Kiswahili mashinini. Jambo hili huwawezesha wakaaji wa mashinani kupata fursa ya kutazama na kuingiliana na vipindi hivyo vya Kiswahili moja kwa moja. Mfano ni matangazo na vipindi kama vile Inspekta Mwala, Papa Shirandula, Habibu, Saida na kadhalika.

Kiswahili pia kinatumika na baadhi ya viongozi kwa kiasi fulani katika mazungumzo yao na hata katika mahojiano kwenye vyombo vya habari vya kimataifa kama vile BBC Uingereza. Viongozi hao pia hutumia Kiswahili katika hotuba zao hasa wanapohutubia wananchi wa nchi jirani za Afrika Mashariki. Kinyume na ilivyokuwa hapo zamani, viongozi na wanajeshi huongea Kiswahili bora kuliko watangulizi wao. Hili ni dhihirisho kuwa Kiswahili kina nafasi ya kuimarika nchini Uganda.

## Namna Kiswahili Kinavyozungumzwa Nchini Uganda

Kuna Kiswahili sanifu na kile kinachozungumzwa mitaani. Kiswahili sanifu ni kile kinachofundishwa na kutahiniwa na hata kutumiwa kwa kiasi katika shughuli rasmi za kiserikali na vyombo vya habari. Kiswahili cha mtaani ni kile kinachozungumzwa katika shughuli za kawaida kuendeleza mawasiliano. Kiswahili hiki kinatambulika na sifa zifuatazo:

- Sarufi haizingatiwi kikamilifu kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:
- *Nina kiti mzuri*
- *Jina yangu iko*
- *Mi apana iko makosa*
- *Twende pande ya Uganda*
- *Apana simama hapa*
- *Wewe apana fikiri*
- *Sema chonataka*

Kutokana na mifano hii, ni wazi kwamba hiki ni Kiswahili cha mkatomkato ambacho hakizingatii upatanisho wa kisarufi. Kwa mfano, matumizi ya neno ‘apana’ hutumiwa kuwasilisha ukanusho na utoaji wa amri.

- Fonolojia ya Kiswahili haizingatiwi ipasavyo kwa mfano,
- *Shamba kutamkwa kama samba*
- *Dhambi kutamkwa kama dambi/zambi*
- *Hapana kutamkwa kama apana*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367

Kwa upande wa msamiati, asilimia kubwa ya maneno hasa nomino ni ya mkopo kutoka lugha za Kiingereza na Kienyeji. Nomino hizo hutoholewa kwa misingi ya mfumo wa lugha za Kibantu kwa mfano maneno kama;

| | | |
|---|---|---|
| Klina | – | Cleaner |
| Vaisi | – | Vice |
| Pulezidenti | – | president n.k. |

- Kuchanganya ndimi au maneno ya Kiswahili, Kiingereza na lugha za kienyeji kuchanganywa katika mazungumzo kwa mfano,

- *Tunataka office messenger na klina ambawo wanajuwa Kiswahili*.
- *Yeye anatoka kwa kyalo-**Yeye anatoka vijijini***
- *Wabbi kwishatoa luggi ya Alexander-**Wezi wameng'oa mlango wa Alexander.***
- Semantiki haizingatiwi. Kwa mfano,
  - *Wewe apana fikiri-* ***Usijali.***
  - *Watu walikuwa wadogo sana-* ***Watu walikuwa wachache mno.***
  - *Leta chupa kavu-* ***Leta chupa tupu.***

Sentensi hizi mbili za mwisho ni tafsiri ya moja kwa moja kutoka lugha ya mama. Katika Luganda, kwa mfano, dhana ya uchache na udogo huwa hazipambanuliwi na kuwasilishwa kwa maneno au istilahi tofauti. Hali kadhalika, dhana ua utupu na ukavu hazipambanuliwi na kuwasilishwa kwa maneno tofauti kama ilivyo katika Kiswahili.

Kiswahili nchini Uganda huzungumzwa namna hivyo kutokana na ukweli kwamba watu wengi hukitumia Kiswahili bila kutilia maanani utaratibu wowote. Sababu ni kuwa hukuna sera au mwongozo maalum wa kuhamasisha watu kuhusu matumizi bara ya Kiswahili.

**Uhusiano wa Kiswahili na Lugha za Kienyeji**

Kiswahili kama asili ya lugha za Kibantu, kinaingiliana sana na lugha zingine za kienyeji kifonolojia, kimofonolojia na kisarufi. Kwa hivyo kulingana na ushahidi wa kiisimu, Kiswahili siyo lugha ya kigeni kama wanavyodai wapinzani wake. Asilimia kubwa ya msamiati unaopatikana katika lugha za kienyeji ni sawa na ule wa Kiswahili. Kwa mfano kwa upande wa msamiati kuna vitenzi kama:

| **Luganda** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Kutega | Kutega |
| Kunywa | Kunywa |
| Kuzaala | Kuzaa |
| Kuziika | Kuzika |
| Kusoma | Kusoma |
| Kuyimba | Kuimba |

Kwa upande wa nomino, kuna maneno kama

| **Luganda** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Mutego | Mtego |
| Kitanda | Kitanda |
| Mukono | Mkono |
| Liiso | Jicho |
| Mukeeka | Mkeka |
| Mumbejja | Mmbeja |

Kuna vielezi kama:

| **Luganda** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Bwerere | Bwerere |
| Juzi | Juzi |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367

**Mifano ya sentensi**

| Kiswahili | Luganda |
|---|---|
| **Ngeli ya KI-VI** | |
| Kitabu hiki ni changu | Ekitabo kino kyaange |
| Kitabu hiki si kizuri | Ekitabo kino si kirungi |
| **Ngeli ya A-WA** | |
| Mtoto anataka kunywa maji | Omwana ayagala kunywa mazzi |
| Watoto wanata kunywa maji | Abaana baagala kunywa mazzi |
| **Ngeli ya U-I** | |
| Mkeka huu ni mpya | Omkeeka guno mupya |
| Mikeka hii ni mipya | Emikeka gino mipya |

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kuwa Kiswahili kina muundo sawa na lugha zingine za Kibantu na kwa hivyo si lugha ngeni kama vile wanavyofikiria wanaopinga lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

**Changamoto Zinazoikabili Lugha ya Kiswahili**

Licha ya uwepo wa Kiswahili nchini Uganda, bado kinakabiliwa na changamoto chungu nzima. Baadhi ya changamoto hizi ni kama ifuatavyo:

- Kuna uhaba wa maandishi /vitabu vya Kiswahili. Vitabu vinavyotegemewa vinatoka nchi jirani hasa nchi ya Kenya na havilengi utamadani wa wananchi wa Uganda. Maandishi yanayopatikana yanalenga jamii na utamaduni wa waandishi husika ambao si wakazi wa nchi ya Uganda. Matekeo ni kwamba mambo yanayoangaziwa hayafungamani moja kwa moja na tajiriba ya jamii za wananchi wa Uganda. Kwa hivyo havina mvuto na ushawishi wa kutosha kwa hadhira lengwa.

- Hakuna majarida/magazeti yanayoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kawaida majarida/magazeti hutoa mchango mkubwa katika kuendeleza umilisi wa lugha. Kutokuwepo kwa vyombo hivi huwanyima wananchi wa Uganda kupata fursa ya kukabiliana na Kiswahili katika maandishi.

- Wananchi wa Uganda wanapendelea Kiingereza na lugha za Kienyeji kuliko Kiswahili. Umilisi wa Kiswahili unachukuliwa kama chombo kisichoweza kumkuza mtu kijamii na kimaendeleo. Kwa upande mwingine, umilisi wa Kiingereza unaaminika kumkuza mtu kwa hali zote kama vile kiuchumi, kielimu, kisiasa, kitabaka miongoni mwa hali zingine. Hali hii inadidimiza/ kufanya Kiswahili kuwa lugha duni isiyotamaniwa na wenyeji wa nchi ya Uganda.

- Wanafunzi wengi wanaosoma na kutahiniwa katika somo la Kiswahili ni wa kutoka nchi jirani na za kigeni kama vile Tanzania, Kenya, Zaire, Rwanda, Burundi na kadhalika. Walimu wanaotegemewa katika kufundisha Kiswahili vyuoni na hata shuleni ni wa kutoka nchi za kigeni hasa Kenya na Tanzania. Jambo hili huchangia katika kuendeleza fikra hasi kuwa Kiswahili hakina nafasi nchini Uganda kwa kuwa kinahusishwa sana na watu wa kutoka nje ya Uganda.

- Hakuna sera mahsusi ya kufuatilia ufundishaji na utumiaji wa Kiswahili katika shule na mawasiliano ya kawaida nchini Uganda. Sera ambazo zipo ni za kimaandishi na kimdomo tu bila utekelezaji. Hali hii inachangia wazo kuwa Kiswahili si muhimu na kukinyima nafasi ya kuimarika ipasavyo.

- Kinyume na vile ilivyo Kenya na Tanzania, Uganda inakosa jamii /wazawa wa Kiswahili wanaoweza kusaidia katika kuikuza na kuiendeleza lugha hiyo. Kwa mfano nchini Kenya na Tanzania kuna lahaja kama vile Kimvita na Kiunguja, zinazohusishwa sana na Kiswahili. Kenya na Tanzania zina historia ndefu ya Kiswahili kuliko nchi ya Uganda.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367

Kiswahili kinakosa msingi wa kurejelewa na kutumiwa kukijenga.

- Kwa kawaida, baadhi ya wananchi wa Uganda bado wana msimamo hasi kuhusu Kiswahili kwa jumla. Wana imani kuwa Kiswahili ni lugha ya vitisho na unyanyasaji, ni lugha inayotumiwa na watu duni na pia ni lugha ya kigeni inayoweza kuzoretesha utamaduni wa raia wa Uganda. Kwa mujibu wa imani yao, umilisi wa Kiswahili si kitu cha kujivunia. Kwa hivyo wananchi wa Uganda hawaoni haja ya kujishughulisha na lugha kama hiyo.

**Mapendekezo**

Kutokana na ukweli kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa, lugha rasmi katika Muungano wa Afrika na *Lingua Franka* katika ukanda wa maziwa makuu, Kiswahili bado kina nafasi kubwa nchini Uganda. Katika enzi hii ya utandawazi wananchi wa Uganda hawana budi kuwa na mwamko wa kikanda na kimataifa kwa kujumuisha Kiswahili kama mojawapo wa lugha zinazoenziwa. Hakuna nafasi kwa wananchi wa Uganda kuendelea kutukuza lugha zao za kienyeji na kupuuza Kiswahili ambayo ni lugha yenye hadhi ya kimataifa. Wasipofanya hivyo wataachwa nyuma kiuchumi na kimaendeleo. Mapendekezo yafuatayo yanaweza kuchangia katika kuinua hadhi ya Kiswahili nchini Uganda na hata nchi zingine zenye nia ya kukijumuisha kama mojawapo wa lugha za kutegemewa kwa mawasiliano.

Kiswahili kitahiniwe kama somo la lazima katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Kwa kuwa mitihani hutiliwa maanani sana katika nchi nyingi ulimwenguni, Kiswahili kikitahiniwa kama somo la lazima, wanafunzi na washika dau wataanza au kulazimika kujishughulisha nacho kama vile wanavyofanya kwa masomo mengine ya lazima.

- Mafunzo maalum yatolewe kwa wafanyikazi wote wa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ili watu wengi waweze kuwasiliana kwa lugha hiyo.

- Kitengo maalum kinachoshughulikia Kiswahili kiundwe katika wizara ya utamaduni ili kuchochea/kuhimiza watu kukienzi Kiswahili.

- Uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili vinavyolenga mazingira na utamaduni wa Uganda uhimizwe ili wananchi waweze kusoma mambo yanayoingiliana na utamaduni wao na hali yao ya maisha.

- Vyombo vya utangazaji vihimizwe kupeperusha vipindi katika lugha ya Kiswahili kama michezo ya kuigiza, matangazo ya kibiashara, na hata nyimbo za Kiswahili kuchezwa mara kawa mara.

- Viongozi kutoka nyanja mbalimbali wahimizwe kuongea Kiswahili sanifu.

- Maandalizi ya makongamano/ warsha kuandaliwa mara kwa mara ili kunufaisha walimu, washika dau na hata wanafunzi wa Kiswahili. Makongamano hayo yanaweza kuandaliwa angalau mara tatu kwa mwaka na kujumuisha wataalamu na wapenzi wote wa lugha ya Kiswahili.

- Sherehe mbalimbali zinazolenga tamaduni za wananchi wa Uganda zinaweza kuandaliwa katika lugha ya Kiswahili. Hali hii inaweza kuchangia katika kuleta wananchi pamoja na kuwafanya kufurahia lugha ya Kiswahili.

- Matangazo ya umma yawekwe katika Kiingereza na Kiswahili kwa mfano, mabango yanayoonyesha ilani, ishara za usafiri, maelezo kuhusu jambo fulani n.k.

- Magazeti yanayosomwa na watu wengi, kwa mfano Monitor na New Vision yanaweza kujaribu angalau mara moja kwa wiki, kuwa na toleo linalohusisha Kiswahili sambamba na Kingereza. Uwepo wa Kiingereza na Kiswahili katika toleo moja unaweza kuchochea msukumo wa kutaka, kwa mfano kuona jinsi ujumbe unaowasilishwa kwa Kingereza unavyopitishwa katika Kiswahili. Kutokana na hali hii, wasomaji wanaweza kujifunza na kuzidisha umilisi wao wa msamiati wa Kiswahili kwa njia rahisi na ya mkato. Magazeti ya lugha za kienyeji nayo pia yanaweza kufanya hivyo hivyo.

- Kufanya juhudi kuhakikisha kwamba kuna hazina ya vitabu vinavyoshughulikia kufanikisha umilisi wa stadi ya kusoma katika Kiswahili kwa watoto wa shule za msingi. Ili kufanikisha jambo hili inafaa kuwa na mpango

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367

kabambe wa kufundisha na kuandaa waandishi watarajiwa kuhusu mbinu mwafaka za kuandika vitabu vya watoto kwa minajili ya kukuza umilisi wa stadi ya kusoma. Wakuza mtaala wa elimu inafaa nao wahusishwe katika harakati hizi.

- Kuunda kitengo maalum cha kukadiria ubora na ufaafu wa vitabu vya Kiswahili vinavyotarajiwa kutumiwa katika ngazi tofauti za elimu nchini. Jambo hili litachangia katika kudhibiti mafunzo ya Kiswahili pamoja na kulinda raia dhidi ya waandishi ghushi ambao nia yao hasa ni kujinufaisha kifedha. Kunaweza kuwa pia na kitengo maalum kinachoshughulikia uundaji wa msamiati na istilahi za Kiswahili. Kitengo hiki kishirikishe wataalam kutoka nchi zote za Afrika Mashariki na hata ulimwenguni ili kuhamasisha watu kupenda lugha ya Kiswahili. Kitengo hiki kijumuishe vile vile watangazaji na washika dau wote wa vyombo vya habari ili kuhakikisha kuwa kuna usawazishaji wa matumizi ya msamiati, istilahi na sarufi sanifu ya Kiswahili.

- Kuandaa warsha maalum mara kwa mara kwa walimu wa shule za msingi ili kuwaelimisha kuhusu mikakati na mbinu za kisasa za kufanikisha umilisi wa stadi ya kusoma. Mbinu hizi zinaweza kuwasaidia pia kuwa na mwelekeo mpya kuhusu umilisi wa stadi za kusoma.

- Kutayarisha mara kwa mara mashindano ya umilisi wa Kiswahili na kuwatuza washindi kwa njia mbalimbali. Jambo hili linaweza kufanyika ikiwa washika dau wahusika wanaweza kutafuta ufadhili kutoka kwa mashirika yenye uwezo kifedha. Mashindano haya yanaweza kufanywa katika viwango mbalimbali vya elimu na kijamii. Mashindano yanaweza kuwa ya ana kwa ana, kupitia vyombo vya habari au katika maandishi.

- Kuwe na haja ya kuwa na sera toshelevu ya lugha ya Kiswahili nchini Uganda kama ilivyo katika nchi ya muungano wa Tanzania ya kushugulikia uzoefu na changamoto za Kiswahili kama ilivyopendekezwa na Msanjila (2009).

## Hitimisho

Haja na sababu za kuimarisha na kukuza Kiswahili nchini Uganda zipo. Sababu za kupinga, na hivyo kuhujumu juhudi za kuendeleza Kiswahili nchini hazina mashiko na zimepitwa na wakati. Changamoto kubwa kwa viongozi husika ni kuwajibika na kujitolea ipasavyo kutekeleza kikamilifu mapendekezo kuhusu Kiswahili yanayotolewa mara kwa mara. Mapendekezo yasipoandamana na vitendo wazi ni kama kiini macho tu.

Kwa mtazamo wa kiisimu, Kiswahili nchini Uganda si lugha ya kigeni. Kimo katika ukoo sawa na lugha za Kibantu za Uganda. Ni lugha inayokua na kupanuka haraka. Inaweza kutumika sambamba na lugha za Kienyeji na ina uwezo mkubwa wa kuchangia katika ukuzaji wa lugha hizo badala ya kuzifisha kama inavyodhaniwa na wapinzani wake. Ni jukumu lisiloepukika la serikali kuhakikisha kwamba inakipa Kiswahili uzito unaostahili kupewa lugha ya taifa. Inapaswa pia kukumbuka kuwa Kiswahili ni nguzo muhimu katika mwamko mpya wa kufufua upya ushirikiano wa kisiasa, kiuchumi na kijamii katika Afrika mashariki na ukanda wa maziwa makuu. Ikiwa Uganda inataka kujinusuru kisiasa na kiuchumi haina budi kufuata mkondo wa nchi jirani kuyaenzi matumizi ya Kiswahili. Kiswahili kitawezesha raia wa Uganda wasiokuwa na uwezo wa kukitumia Kiingereza au Kifaransa kuwasiliana kwa urahisi na wenzao katika ukanda wa Afrika mashariki na eneo la maziwa makuu.

Huu ni wakati mwafaka kwa vyombo vya dola vilivyo na jukumu la utekelezaji wa sera kuonyesha kwa vitendo kwamba vinayo nia ya kukuza Kiswahili nchini Uganda. La sivyo tabia endelelezi ya kukawilisha utekelezaji wa mapendekezo mbalimbali yanayoangazia Kiswahili huenda ikafasiriwa kuwa njama ya kuendeleza kisirisiri vita baridi dhidi ya Kiswahili.

## MAREJELEO


Abdallah, K. (1977). *The Liberation of Swahili from European Appropriation*. Nairobi. East African Literature Bureau.

Chimera, R. (1998*). Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: N.U.P


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.367

Kihore, Y. M. (1983). 'Nafasi ya Kiswahili Barani Afrika,' katika *MULIKA* Nambari 15, uk. 32-39

Mazrui, A. A., & Mazrui, A. M. (1995*). Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language*. Nairobi: E.AE.P.

Mbaabu, I. (1978). *New Horizons in Kiswahili*. Nairobi: KLB.

Mbaabu, I. (1995). "Linguistic and Cultural Dependency in Africa," katika *BARAGUMU*, Jizuu la 2 Namb. 1-2 uk. 72-86.

Ministry of Education and Sports (2012). *Primary Seven Curriculum*. Kampala. National Curriculum Centre.

Msanjila, Y.P. (1997). "Towards A Policy on the Use of Kiswahili in Africa," katika *Kiswahili*. Juzuu la 60. Uk. 61-67.

Msanjila, Y. P. (2003). "Kushuka kwa Hadhi ya Lugha za Jamii Nchini Tanzania," in Nordic Journal of African Studies12 (3). 296–309

Msanjila, Y.P. (2009). "Haja ya Kuwa na Sera Tosherevu ya Lugha Tanzania: Uzoefu na Changamoto", Katika Mulika.28

Whitely, W.H. (1969). *Swahili: The Rise of the Swahili Language*. Methuen & Co. Ltd., London.

Whitely, W. H. (1971). "Some Factors Influencing Language Policies in Estern Africa" in Rubin Joan (1971) *Can Language be Planned?* The University Press of Hawii.